# Mbinu Mbalimbali za Kutathmini Tafsiri

*Pendo S. Malangwa*

*Ikisiri*

Makala haya yanajadili mbinu mbalimbali za kutathmini tafsiri katika muktadha wa tafsiri za Kiswahili na lugha nyingine za Tanzania. Madai makuu ya makala haya ni kwamba tafsiri hufanyiwa tathmini katika hatua zake mbalimbali. Tathmini katika tafsiri[1] inaweza kufanyika mwanzo (yaani, kabla ya kuanza kutafsiri), katikati ya mchakato wa kutafsiri na mwishoni (yaani, baada ya tafsiri kufanyika). Tathmini inaweza kufanyika kwa kutumia mbinu ya kulinganisha matini, kufanya tafsiri rejeshi, mbinu ya kupima uelewa, kupima usomekaji na kupima uasili. Madai ya makala haya ni kwamba mbinu hizi hutumika kutegemeana na aina ya tathmini inayofanyika. Aidha, mbinu zaidi ya moja zinaweza kutumika katika kutathmini tafsiri moja. Kupitia tathmini, tafsiri zimekuwa zikiboreshwa kila mara, na hata wanazuoni wamekuwa wakiibua mikakati na mbinu mpya za kuboresha mchakato wa kutafsiri.

## 1.0 Utangulizi

Kila jambo au zoezi lenye tija hufaa kufanyiwa tathmini ili kujua kiwango cha ubora na/au upungufu wake. Wakati mwingine tathmini inaweza kusaidia kujua ikiwa welekeo wa zoezi hilo ni chanya au la (na hii hufanyika katikati ya zoezi linaloendelea). Tathmini pia inaweza kufanyika mwanzoni mwa zoezi au jambo husika ili kuelewa manufaa, ugumu na/au uwezekano wa jambo hilo kufanyika, gharama za kutekeleza jambo hilo, na kadhalika. Tafsiri ni zoezi lenye tija katika jamii kutokana na ukweli kwamba imesaidia kuwaunganisha watu wa mataifa mbalimbali wanaozungumza lugha tofauti (taz. Walibora, 2001 na Malangwa, 2008). Tafsiri pia inasaidia kueneza maarifa, utamaduni, ujuzi na elimu kutoka jamii moja kwenda nyingine (taz. Mwansoko na wenzie, 2006). Kwa hiyo, ni vyema tafsiri, kama zoezi au zao, kufanyiwa tathmini kama ilivyoelezwa hapo awali. Tathmini ya tafsiri husaidia kuboresha zoezi la tafsiri na/ au zao la tafsiri.

Tathmini ya tafsiri inaweza kufanywa na mzungumzaji mzawa, mhakiki wa tafsiri, mhakiki wa matini, mshauri wa masuala ya tafsiri, mfasiri mwenyewe, mteja aliyewasilisha matini inayofasiriwa au mtaalamu katika uwanja husika. Kwa mfano, mfasiri kwa kawaida hukagua na kutathmini tafsiri yake mara kwa mara wakati wa zoezi la uhawilishaji na mwishoni mwa zoezi hilo. Wakati mwingine, kama kuna mshauri wa masuala ya tafsiri, anaweza kuonwa ili kutathmini tafsiri husika baada ya mfasiri kukamilisha zoezi lake. Mshauri wa tafsiri hujikita katika kuangalia masuala ya kanuni na mbinu za tafsiri kama

[1] Kutafsiri pia kuna maana ya kufasiri. Kwa hiyo, maneno hayo yatatumika yakiwa na maana sawa.

zimezingatiwa na kama zimetumika kwa usahihi au kama zimekiukwa. Halikadhalika, mshauri wa tafsiri anaweza kumwelekeza mfasiri kuhusu mbinu mbalimbali za kutathmini tafsiri. Mfasiri atafaidika sana ikiwa atafanya kazi bega kwa bega na mshauri wa masuala ya tafsiri. Ni vyema tukasisitiza hapa kwamba, tafsiri yoyote inaweza kuwa bora iwapo watu mbalimbali watashirikishwa katika kuitathmini. Bielsa na Bassnett (2009) wanasisitiza kwamba ni vyema tafsiri yoyote ikapitishwa katika jozi nyingine za macho kabla haijachapishwa kwa mara ya mwisho. Hii itasaidia kuhakiki usahihi wa taarifa muhimu kama vile takwimu, tarehe, maudhui na data nyingine. Katika makala haya tutaziangalia mbinu mbalimbali za kutathmini tafsiri katika muktadha wa tafsiri za Kiswahili na lugha nyingine za Tanzania. Kwa misingi hiyo tunaanza na kuainisha matini lengwa, ambazo ndizo zao la tafsiri na ambazo ndizo hutathminiwa; kisha tunaabiri mbinu mbalimbali za kufanya tathmini.

## 2.0 Aina za Matini Lengwa Zinazoweza Kufanyiwa Tathmini

Kuna aina kuu mbili za Matini Lengwa (ML) zinazoweza kufanyiwa tathmini. Kwanza, kuna ML ambazo zipo katika mchakato wa kutafsiri. Matini hizi ni zile ambazo bado zinafanyiwa kazi na hazijamfikia msomaji husika wa lugha lengwa (LL). Matini hizi hufanyiwa tathmini ili kubaini kama malengo ya tafsiri hiyo yamefikiwa au la. Aidha, tathmini ya matini hizi hufanywa na mfasiri ili kujiridhisha na kazi aliyoifanya au mtu mwingine hutathmini tafsiri husika kwa lengo la kumshauri mfasiri juu ya namna nzuri ya kuboresha tafsiri yake. Larson (1984) anafafanua kwamba mfasiri daima anatamani kwamba matokeo ya kazi yake yawe na ubora wa kiwango cha juu. Mfasiri anaweza kubaini ubora wa kazi yake kwa kufanya tathmini katika hatua mbalimbali za zoezi la kutafsiri na mwishoni mwa zoezi hilo. Ikiwa mfasiri atapuuza zoezi la kutathmini tafsiri yake basi, tafsiri yake pia haitakuwa na ubora anaoutamani au unaotarajiwa. Kadiri mfasiri anavyofanya tathmini ya kazi zake na kupata maoni, ndivyo anavyoboresha utendaji wake siku hadi siku na matokeo yake anakuwa mfasiri bora. Kwa kuneneleza yaliyoelezwa hapo, tathmini ya matini za kundi hili inaweza kufanywa na mzungumzaji mzawa, mhakiki wa tafsiri, mhakiki wa matini, mfasiri mwenyewe, mteja aliyewasilisha matini inayofasiriwa au mtaalamu katika uwanja huu. Hapa mtu anayefanya tathmini hufanya hivyo kwa ama kuilinganisha matini ya lugha lengwa (MLL) na ile matini lugha chanzi (MLC) au kuisoma matini kwa lengo la kutathmini masuala ya uasili.

Kundi la pili la ML linahusisha matini ambazo tayari ziko mikononi mwa mtumiaji wa LL. Matini hizi hufanyiwa tathmini ili kubaini upungufu au ubora uliopo kwa lengo la kuboresha zaidi tafsiri zinazofuata au zitakazofasiriwa

katika LL. Mathalani, wafasiri wengi wa matini za kidini, kama vile, nyimbo za dini, Biblia na Kuran, baada ya tafsiri zao kutumika kwa muda fulani, huweza kuzirejea kwa lengo la kuzitathmini na kuona upungufu uliopo ili kuziboresha. Kwa kawaida, tathmini ya matini hizi inaweza kufanywa na mfasiri mwenyewe, mwanataaluma katika uwanja wa tafsiri, na kadhalika. Hapa mtu anayetathmini tafsiri hufanya hivyo kwa kuilinganisha tafsiri na matini ya lugha chanzi (MLC). Baada ya kubaini upungufu fulani, mfasiri huanza kuandaa toleo lingine la MLL. Halikadhalika, matini za kundi hili zinaweza kufanyiwa tathmini na wataalamu wa uwanja wa tafsiri ili kubaini kasoro au udhaifu unaojitokeza katika kazi hizi kwa lengo la kuboresha nadharia ya tafsiri. Kwa mfano, wanafunzi wengi wa tafsiri katika lugha mbalimbali wamekuwa wakifanya tathmini ya tafsiri mbalimbali na kupendekeza mbinu bora za kuboresha mchakato wa tafsiri. Mfano wa utafiti uliofanyika katika Kiswahili kwa lengo la kutathmini tafsiri na kupendekeza mbinu au mikakati ya uboreshaji wa tafsiri ni kama zile za Mutasa (1999), King'ei (2002), Malangwa (2005&2010), Fupi (2010) na Pembe (2010). Kwa hiyo, zoezi la kutathmini tafsiri ni muhimu sana katika kuboresha nadharia ya tafsiri na tafsiri zinazotolewa siku hadi siku.

## 3.0 Mbinu za Kutathmini Tafsiri

Wataalamu mbalimbali wa tafsiri, kama vile Larson (1984) na Hosseini (2008) wanadai kwamba kuna mbinu tano (5) ambazo hutumika katika kutathmini tafsiri. Lakini uzoefu unaonesha kwamba kuna mbinu kuu sita ambazo hutumiwa na wafasiri, washauri wa tafsiri, wahakiki wa tafsiri, wahakiki wa matini, wafasiri wenyewe, na kadhalika. Mbinu hizo ni kulinganisha matini, kupima uasili, kupima uelewekaji, kupima usomekaji, kufanya rejeshi na kupima ulinganifu. Makala haya yatajadili mbinu hizi kwa kurejea hali halisi katika tafsiri za Kiswahili.

### 3.1 Kulinganisha Matini

Hii ni mbinu kongwe na hutumiwa na wafasiri na wataalamu wengi wa tafsiri wanapotathmini au kupima tafsiri mbalimbali. Kwa kawaida, mfasiri anapokamilisha zoezi la kutafsiri matini husika, huchukua tafsiri yake na kuilinganisha na MLC. Zoezi hili hufanyika kwa malengo makuu mawili: kwanza, mfasiri hulinganisha matini zake ili kuona kama amefanikiwa kuingiza taarifa zote za matini chanzi (MC); pili, baada ya kuhakiki taarifa mfasiri hulazimika pia kuangalia ikiwa amefanikiwa kushughulikia kikamilifu vipengele vyote vya kimuundo. Hapa huhakiki pia kuona kama ameingiza taarifa nyingine za ziada ambazo hazikuwepo katika MLC. Wakati mwingine, mfasiri anaweza kumpatia msomaji mwingine ambaye anazifahamu lugha zote mbili, lugha ya MC na ile ya ML, ili atoe maoni kuhusiana na tafsiri

iliyotolewa. Mathalani, mfasiri au mtu anayetathmini tafsiri anaweza kulinganisha matini zifuatazo:

**Mfano 1**:

| Matini ya LC | Matini ya LL |
|---|---|
| Get a Digital ID. In order to sign a Microsoft Office document, you need a digital ID. You have two options for getting a digital ID: Get a digital ID from a Microsoft partner. If you use a digital ID from a Microsoft partner, other people will be able to verify the authenticity of your signature. Create your own digital ID. If you create your own digital ID, other people will not be able to verify the authenticity of your signature. You will be able to verify the authenticity of your signature, **but only on this computer**. | Pata Kitambulisho Dijito. Ili kusaini waraka wa *Microsoft Office*, unahitaji kitambulisho Dijito. Una machaguo mawili kwa ajili ya kupata kitambulisho Dijito: Pata kitambulisho Dijito kutoka kwa mbia wa Microsoft. Kama unatumia kitambulisho Dijito kutoka kwa mbia wa Microsoft, watu wengine wataweza kuhakiki uhalali wa saini yako. Unda kitambulisho Dijito chako mwenyewe. Kama unaunda kitambulisho Dijito chako mwenyewe, watu wengine hawataweza kuhakiki uhalali wa saini yako. Utaweza kuhahiki uhalali wa saini yako. |

**Chanzo cha data**: *Tafsiri za programu za kompyuta za Microsoft, 2008*

Katika kutathmini tafsiri iliyotolewa kwa kuilinganisha na MC, mfasiri au mhakiki wa tafsiri hii atalazimika kupitia mstari kwa mstari ili kuhakiki kwamba taarifa zote zimehawilishwa. Mathalani, katika mfano huu mstari unaosomeka ... ***but only on this computer***, umesahaulika au umedondoshwa kwenye MLL. Kwa hiyo, kama tafsiri hii itatolewa pasipo kufanyiwa uhakiki, itakuwa na upungufu wa taarifa muhimu za MLC na hivyo kumpotosha msomaji wa LL. Halikadhalika, baadhi ya wafasiri wa Biblia katika lugha mbalimbali, kikiwamo Kiingereza, wangefanya uhakiki wa kutosha kuhusu tafsiri zao, wangeweza kubaini kwamba mstari wa Yohana 5:4 umesahaulika katika tafsiri zao. Tazama ulinganishi ufuatao:

**Mfano 2**:

| | |
|---|---|
| | **Tafsiri ya Kiingereza** **(*The Holy Bible*)** |
| (a) | 5After this, Jesus went to Jerusalem for religious festival. 2Near the Sheep Gate in Jerusalem there is a pool with five porches; in Hebrew it is called Bethzatha. 3A large crowd of sick people were lying on the porches- the blind, the lame, and the paralylized. 5A man was there who had been sick for thirty-eight years. ... |
| (b ) | **Tafsiri ya Kijita** **(*Indagano Inya:ya*)** |
| | 5Wejire ebyo byawa, nigabao amarya ga Bayahudi. Yesu narinya mu Yersalemi. 2Mbe mu Yerusalemi kwirango rinu ryatogwaga Rya JIna:ma, ririko ritanga, rinu ryatogwaga mu Cieburania, Betesida, ririo na biyumba bita:nu. 3Mwibyo bama:magamo ecise ca barwae, baofu na barema na bakombo:kire. 5Ariga ario omu:nu arwae, amarire myaka makumi gasatu neta:nu nesatu(38). ... |
| (c) | **Tafsiri ya Kiswahili** **(*Biblia Maandiko Matakatifu*)** |
| | 5 1Baada ya hayo palikuwa na sikukuu ya Wayahudi; naye Yesu akakwea kwenda |

| | |
|---|---|
| | Yerusalemu. 2Na huko Yerusalemu penye mlango wa kondoo pana birika, iitwayo kwa Kiebrania Bethzatha, nayo ina matao matano. 3Ndani ya hayo jamii kubwa ya wagonjwa walikuwa wamelala, vipofu, viwete, nao waliopooza, [***wakingoja maji yachemke. 4Kwa maana kuna wakati ambapo malaika hushuka, akaingia katika ile birika, akayatibua maji. Basi yeye aliyeingia wa kwanza baada ya maji kutibuliwa, akapona ugonjwa wote uliokuwa umempata.***] 5Na hapa palikuwa na mtu, ambaye amekuwa hawezi muda wa miaka thelathini na nane. … |
| (d) | **Tafsiri ya Kinyakyusa** <br> (***Tesitamenti Umpya***) |
| | 5 1. Pańuma pali sịsịsị po kilinkujapo ikyaka kimo kya ba-Juta. Jope na-Jesu alinkufyuka alinkubuka mụ-Jelusalemu. 2. Lelo mụ-Jelusalemu pakipata kya nosị, po kilịpo ikisịba iki ingamụ jake mụnjobelo ja ba-Juta bịkuti jo Betesita. Kili namatembe masano. 3. Mo bālambalele abandu bịngị fịjo ababịne nabafwamaso nāba bịkukwema nāba balalịle umbili. aba bāgulilaga amisi ukusụkanika. **4.** [***Namaga ugwandumị āsụlụkaga mbusịkụ mbusịkụ alikwịngila nkịsịba alikungajụnganya amisi. Lelo uju linga ātalịlepo pakwịngila mmisi bogafụmịle. pakujụnganika, jo alinkubumbuluka indamwa josa ịtolo ijị linga āli najo.***] 5. Lelo ālịpo papo umụndu uju āgonịle nindamwa jake ifyinja amalongo matatu na lwele. … |

**Chanzo**: *Biblia Injili ya Yohana 5:1-5*

Katika sampuli ya tafsiri hizi zote inaonekana kwamba tafsiri ya Kiingereza na Kijita haikufanyiwa tathmini au imefanyiwa tathmini lakini si kwa umakini unaotakiwa. Sababu za kudondoshwa kwa taarifa zilizopo katika mstari wa nne hazikupatikana lakini inawezekana zikawa zimesababishwa na baadhi ya wafasiri kuupuuza mstari huo au kusahaulika kwa mstari huo wakati wa zoezi la kufasiri. Kwa upande wa tafsiri ya Kinyakyusa na Kiswahili, mstari wa nne umejitokeza katika matini lengwa. Pengine tudokeze tu hapa kwamba, tafsiri nyingi za maandiko ya kidini zinatokana na matini za tafsiri katika lugha nyingine. Wafasiri wengi wa maandiko haya hawakufanikiwa kupata matini chanzi ili wafasiri kutoka katika lugha chanzi. Hii inaweza kusababishwa na ama kukosekana kwa matini za lugha chanzi, au wafasiri kutofahamu lugha ya matini chanzi na hivyo kuamua kutumia matini za kwenda katika lugha zao. Hata hivyo, tatizo lililotokea katika tafsiri hizi ni la kizembe kwani wafasiri katika Kiingereza na Kijita wangeweza kufanya utafiti ili kuhakiki matini zao. Ni vyema mfasiri anapogundua tatizo kwenye tafsiri yake alifanyie uchunguzi kabla ya kuichapa tafsiri yake.

Inapendekezwa na wataalamu wengi kwamba ni vyema mfasiri aichape kazi yake na aiweke kwenye matini yenye nafasi maradufu baina ya mstari mmoja na mwingine ili kumwezesha mhakiki kuandika maoni yake ndani ya matini hiyo. Maoni hayo yanaweza kujumuisha sehemu zilizosahaulika au kudondoshwa pamoja na taarifa za ziada zilizoongezwa kwenye MLL au zilizopotoshwa. Larson (1984) anafafanua kwamba mfasiri katika zoezi lake la uhawilishaji hutathmini tafsiri yake kwa kuilinganisha na MLC ili kujua welekeo wa zoezi lake. Hata baada ya zoezi la kutafsiri, mfasiri huihakiki tafsiri yake yote kwa kuilinganisha na matini chanzi kabla ya ama kumpatia msomaji

mwingine au mteja wake. Kwa kufanya hivyo, mfasiri hutoa tafsiri bora ambayo hata yeye mwenyewe huifurahia.

## 3.2 Kupima Uasili

Mchakato wa kupima uasili katika tafsiri iliyotolewa hufanyika kwa kuitazama tafsiri peke yake, pasipo kuiwianisha na MLC. Wataalam wa masuala ya tafsiri, kama vile Nida na Taber (1982), wanashauri kwamba tafsiri haipaswi kuwa na vionjo vyovyote vya lugha chanzi. Hivyo, tafsiri inayotolewa inapaswa isomeke kana kwamba imendikwa katika lugha lengwa hiyo. Mtu mwingine, mbali na mfasiri, hupewa matini ya tafsiri (yaani, matini ya lugha lengwa) ili aisome na kurekebisha makosa yanayojitokeza hasa katika suala la uasili. Hatua ya kwanza katika kupima uasili ni kuisoma rasimu yote ya tafsiri. Hatua hii ni muhimu katika kuangalia mtiririko wa tafsiri hiyo pamoja na ujumbe unaowasilishwa kama unaeleweka au la. Baadhi ya wasomaji hupenda kusoma kwa sauti na wengine kimyakimya. Kwa kawaida, msomaji wa tafsiri husoma tafsiri huku akiwa na kalamu ya risasi mkononi mwake ili kupigia mistari au kuwekea alama sehemu ambazo hazisomeki vizuri au hazisomeki katika uasili. Baada ya kusoma yote, msomaji wa tafsiri hurejea tena kusoma kwenye sehemu alizozipigia mistari. Katika kusoma sehemu hizi, anaweza kuandika maoni ndani ya matini ya tafsiri hiyo au kwenye karatasi nyingine ya pembeni. Baadaye, msomaji anapaswa kurejea tena kuisoma tafsiri nzima ili kuona kama anaweza kutoa maoni mengine zaidi kuhusu namna ya kuboresha tafsiri hiyo.

Kwa kawaida, mhakiki anashauriwa kutoa mapendekezo ya kuboresha na siyo kukosoa tu. Wahakiki ni watu muhimu sana kwa mfasiri katika kuboresha tafsiri yake, hasa kama mfasiri atatumia maoni hayo kwa uangalifu. Wakati mwingine, mhakiki wa uasili kama ataona matatizo makubwa katika tafsiri inayohusika, anaweza kuomba kuiona MLC ili asome kwa kulinganisha na MLL (Hosseini, 2008), na hili linawezekana tu kwa wasomaji wanaozifahamu lugha zote mbili.

Kama mada hii inavyojifafanua, lengo kuu la kutathmini tafsiri ni kuona uasili uliomo katika vipengele vya kimuundo pamoja na mtindo wa uwasilishaji. Inapendekezwa na wataalamu kama Larson (1984) kwamba ni vyema wanaotathmini tafsiri kwa kuangalia uasili na usomekaji wakawa wahakiki waliobobea au wenye ujuzi wa kuandika katika lugha lengwa (LL). Halikadhalika, wahakiki wanaopewa kutathmini tafsiri kwa kuangalia uasili wanapaswa kuwa watu wanaopenda kusoma kwa lengo la kupima uasili na usahihi, na hatimaye kumpatia mfasiri maoni ya kuboresha kazi yake. Wahakiki wengi wa uasili husoma tafsiri wakipendekeza au kuonesha namna nzuri ya kurekebisha miundo na mitindo ya tafsiri ili isomeka kana kwamba imeandikwa katika LL. Miundo yoyote yenye ukiushi wa aina yoyote inapaswa

kurekebishwa kabla ya kutolewa kwa rasimu ya mwisho ya tafsiri. Hebu tutazame tafsiri ifuatayo ya mkataba wa kibiashara:

**Mfano 3**:

| | **Kabla ya tathmini** | **Baada ya Tathmini** |
|---|---|---|
| | Shughuli zote za uuzaji wa kujitangaza zinazofanywa na msambazaji wa badhaa za aina yoyote lazima ziwe zimeidhinishwa na mhusika mkuu ambaye ana haki yote na busara zote za kukataza shughuli hiyo. Gharama zote za utangazaji, utafuta soko na shughuli za uuzaji wa kujitangaza unaofanywa na mhsika mkuu ndani ya eneo zitachangiwa, isipokuwa kama itakubalika vinginevyo na msambazaji na mhusika mkuu. | Shughuli zote za kutangaza biashara za aina yoyote zinazofanywa na msambazaji wa bidhaa lazima ziwe zimeidhinishwa na mhusika mkuu ambaye ana haki ya kukataza shughuli hiyo kwa busara zake. Gharama zote za kutangaza, kutafuta soko na shughuli za matangazo ya biashara zinazofanywa na mhusika mkuu ndani ya eneo la biashara zitagharimiwa kwa ubia isipokuwa kama mhusika na msambazaji watakubaliana vinginevyo. |

**Chanzo:** *Sehemu ndogo ya mkataba uliowasilishwa TUKI, 2008 kwa ajili ya tafsiri*

Kwa kuangalia tafsiri hizi, msomaji atagundua kwamba tafsiri iliyotolewa awali, kabla ya zoezi la kupima uasili, inaweza kumdokeza msomaji kuwa hii ni tafsiri na inamfanya msomaji asielewe maudhui ya matini hiyo. Wengi wataafiki kwamba tafsiri baada ya tathmini inasomeka katika uasili na miundo yake ina uasili wa LL. Tafsiri yoyote haipaswi kusomeka na kuonekana kwamba ni tafsiri kutoka lugha fulani. Daima kazi ya tafsiri inapaswa kusomeka katika uasili ili kuwasaidia wasomaji wa LL wajisikie kwamba kazi hiyo ni yao na imeandikwa na mzungumzaji mzawa. Mhakiki anaweza kuwa mahiri wa lugha zote mbili, LL na LC, lakini anapaswa pia kuwa na ujuzi wa kuirekebisha tafsiri yake ili iwasilishe ujumbe unaoeleweka kwa wasomaji wa LL.

Kama itaonekana kwamba tafsiri iliyotolewa haisomeki kwa uasili na haiwasilishi ujumbe wa MLC, basi mhakiki wa tafsiri hiyo anaweza kutoa mapendekezo fulani ambayo yanaweza kufanyika kwa lengo la kuboresha tafsiri hiyo. Moja ya mapendekezo hayo inaweza kuwa mfasiri awasilishe kwa msomaji matini ya LC sambamba na ile ya LL ili apewe maoni yatakayoboresha tafsiri yake. Wakati mwingine mhakiki anaweza kupendekeza tafsiri ifanyike tena. Mfasiri kama hajaridhika na maoni yaliyotolewa na msomaji wa kwanza anaweza kutafuta msomaji wa pili au zaidi ili kupata maoni yatakayomsaidia kuboresha tafsiri yake. Katika nadharia za tafsiri inashauriwa kwamba kadiri mfasiri anavyopata maoni kutoka kwa wahakiki mbalimbali ndivyo anavyoboresha tafsiri yake na kuifanya isomeke kana kwamba imeandikwa katika lugha lengwa (Larson, 1984). Ni vyema tafsiri yoyote ikawa na uasili wa LL, isisomeke kama tafsiri.

### 3.3 Kupima Uelewekaji

Lengo kuu la kupima uelewekaji ni kuona kama maudhui ya tafsiri yanaeleweka kwa wasomaji wa LL au la. Mfasiri au mtu mwingine mwenye ujuzi wa kupima uelewekaji anaweza kutathmini tafsiri katika kipengele hiki cha uelewekaji. Kama mfasiri mwenyewe atafanya tathmini hii anapaswa kuwa mwangalifu ili kuepuka kujitetea sana au kutetea tafsiri yake kwa kutoa ufafanuzi. Anapaswa ajitahidi kupima uelewekaji wa maudhui yake kwa wasomaji wa LL. Hata hivyo, inapendekezwa kwamba mtu mwingine, tofauti na mfasiri, afanye tathmini hii. Mtu huyo anapaswa kuwa na uhusiano mzuri na watu anaowashirikisha katika kutathmini tafsiri hiyo na anapaswa kuwa mtu aliyesomea kuhakiki au kutathmini tafsiri. Anapaswa kuwa na ujuzi wa kusikiliza na kuandika maoni yanayotolewa na wazungumzaji wa LL.

Watu wanaoshirikishwa katika mchakato wa kupima uelewekaji wanapaswa kuwa vijana, watu wa makamo ya kati na wazee wanaozungumza LL. Watu hawa wanapaswa kutoka katika makundi mbalimbali ya jamii, wasomi na wasio wasomi, wenye ujuzi wa kusoma na/au wanaosoma. Ikiwa tafsiri hiyo imekusudiwa kutumika katika muktadha maalumu, basi watu walio katika eneo hilo ndio watakaoshirikishwa katika kutathmini tafsiri hiyo. Mathalani, kwa tafsiri za uwanja wa sheria, mhakiki anapaswa kuwashirikisha wanasheria au watu wanaosomea sheria ili kupima usahihi wa maudhui yanayowasilishwa. Watu wanaoshirikishwa katika kutathmini tafsiri wanapaswa kuwekwa katika mazingira tulivu na wawe na muda wa kutosha. Halikadhalika, wanapaswa kuonesha utayari wa kushiriki na kusaidia kuboresha tafsiri. Mhakiki anapaswa kuwaelewesha washiriki kwamba lengo la kupima uelewekaji siyo kumpima yeye bali ni kupima tafsiri kama inaeleweka. Hii siyo jaribio la kupima uwezo wa kuelewa, wala si zoezi la kupima uwezo wake wa kukumbuka na wala siyo zoezi la kupima uwezo wake wa kujibu maswali vizuri. Zoezi hili ni la kupima tafsiri ili kuona kama inahitaji kuboreshwa.

Njia inayotumika katika kupima uelewekaji ni kuwapatia matini ya tafsiri wazungumzaji wa LL ili waisome na kusimulia maudhui yanayowasilishwa. Mhakiki anapaswa kuchagua sehemu ndogo[2] ya matini ambayo ndio kiini cha matini na kuipeleka kwa watu anaowashirikisha katika kupima uelewekaji. Halikadhalika, mfasiri anaweza kuwauliza maswali ya uelewa ili aweze kuboresha tafsiri yake. Maswali yanayoweza kuulizwa ni pamoja na:

---

[2] Lengo kuu la kuteua sehemu ndogo ni kuokoa muda. Uteuzi wa sehemu ndogo unapendekezwa hasa kwa matini ambazo ni ndefu. Hivyo, mfasiri anaweza kuteua sura moja au aya chache ambazo zinabeba wazo kuu la matini na kuipeleka katika zoezi la tathmini. Lakini kama matini ni ndogo, yenye kurasa chache, mhakiki anashauriwa kuiwasilisha matini nzima ili kutathminiwa.

(a) Je, andiko hili linahusu nini?
(b) Aliyeandika aya hii anakusudia isomwe na vijana au wazee, wanawake au watoto?
(c) Anazungumza na nani? Watoto, wazee, vijana, wanawake au wanaume?

Maswali kama haya yanaweza kuandaliwa kutegemeana na aina ya matini inayoshughulikiwa. Majibu yanaweza kuwa ya kufafanua maudhui, kukosoa lugha iliyotumika au kufafanua mtindo wa uwasilishaji wa maudhui. Mfano wa matini inayoweza kupimwa uelewekaji wake ni kama ifuatayo:

**Mfano 4**:

*Utandawazi ni dhana ambayo imeenea kwa kasi kama moto wa nyika katika hii miaka ya karibuni. Ni dhana ambayo imewateka wasomi, wanasiasa, wachumi na waandishi wa habari barani Afrika na kuwaganda mgongoni kama yule mzee aliyempanda Sindbad katika ngano za kale kisha akakataa kushuka. Utumizi wa dhana hii umekuwa fasheni miongoni mwa watu wengi barani Afrika katika kipindi ambacho duniani kote watu ambao wameshamaizi uhalisia wa mfumo wa uhusiano unaoimarishwa na dhana hiyo wamejitokeza kwa wingi kuupinga kwa nguvu. Maandamano ya kwanza yaliyofanyika kuupinga utandawazi yaliandaliwa huko Mexico mnamo mwaka 1994. Baada ya hapo yalifanyika mengine kuanzia mwaka 1999 huko Seattle, na baada ya hapo yameendelea kufanyika... (Chachage, 2004 :1).*

Maswali yanayoweza kutumika kupima uelewekaji wa maudhui ni kama haya:
(i) Je, utandawazi umeeneaje duniani?
(ii) Watu gani Afrika huuchukulia utandawazi kama fasheni?
(iii) Je, utandawazi bado unakubalika duniani?

Wakati wa mahojiano, mhakiki anapaswa kuandika au kutunza kumbukumbu za yale yote yanayozungumzwa. Anaweza ama kuandika au kurekodi kwa kutumia vifaa kama vile redio, simu au kamera ili mfasiri na mhakiki waweze kurejea kwa urahisi wakati wa kuboresha tafsiri. Aidha, kila mshiriki wa zoezi hili anapaswa kupewa tafsiri iliyochapwa na yenye nafasi maradufu baina ya mistari. Ataisoma na kutoa maoni ndani ya tafsiri hiyo na/au kwenye karatasi nyingine pembeni ikibidi.

Kwa ujumla, kuna michakato mikuu miwili ya kutathmini uelewekaji wa matini ya tafsiri. Kwanza, ni kuwapatia wasomaji tafsiri nzima au sehemu ndogo ya tafsiri ili wasome na kutoa maoni. Pili ni kuwauliza maswali yanayohusu maudhui ya matini au masuala ya mtindo. Mhakiki wa tafsiri anapaswa kwenda hatua kwa hatua, akiwapatia wasomaji wake muda wa kutosha wa kusoma au kufanya uchambuzi.

## 3.4 Kupima Usomekaji

Mbinu hii inawiana na ile ya kupima uasili. Katika mbinu hii, mfasiri au mhakiki anaweza kuendesha zoezi la kupima tafsiri husika ikiwa inasikika vyema masikioni mwa msikilizaji na kama ina mtiriko unaokubalika katika LL. Ili kukamilisha zoezi hili, watu au mtu mwingine (kwa kawaida awe mmilisi au mahiri wa LL) huombwa kusoma kwa sauti sehemu ndogo ya tafsiri, hasa kama tafsiri husika ni ndefu. Sehemu inayoteuliwa kupima usomekaji inapaswa kuwa inayojitosheleza kimaana au kizio kizima cha tafsiri (mf. aya, sura au sehemu). Wakati mtu huyo akisoma, mhakiki wa tafsiri anapaswa kuwa na nakala ya tafsiri hiyo akifuatilia na kuweka alama katika sehemu ambazo zina matatizo, msomaji anakwamakwama, sehemu zenye taarifa isiyo kamili, na kadhalika. Anapaswa pia kuwekea alama sehemu ambazo msomaji anasoma kwa kurudiarudia kwani hali hii inaashiria kwamba kuna matatizo ya usomekaji wa matini.

Mtu anayetathmini tafsiri husika hapaswi kumwuliza msomaji maswali ya kuumiza kihisia. Anapaswa kufuatilia huku akiweka alama kimyakimya, akiandika mapendekezo au hata kuandika maelezo pembezoni mwa kurasa za matini. Kama atapata nafasi ya kutosha, anaweza hata kuandika sababu za ugumu uliojitokeza. Larson (1984) anatahadharisha kwamba wale wanaopima usomekaji na uelewekaji wa taarifa za matini ya tafsiri wanapaswa pia kuangalia sehemu zilizoshehenezwa taarifa. Tafsiri yoyote itasomeka vizuri kama itaandikwa vizuri. Mawazo haya yameungwa mkono na Hosseini (2008) ambaye pia anafafanua kwamba tafsiri bora itasomeka kwa namna ambayo haitamchosha msomaji kwa taarifa za kujirudiarudia. Hebu tazama matini ifuatayo:

**Mfano 5**:

> *Ni ukweli usipingika kuwa uzoefu wa madawa madawa ya aina yoyote haufai. Ni tatizo kubwa kwa sababu ni aina ya utumwa. Uzoefu wa madawa kama pombe, tumbaku (nicotine),* ***caffeine*** *(kileo kinachopatikana katika buni-kahawa na cocoa), ama yale madawa ya kulevya kama bhangi,* ***cocaine*** *na kadhalika .ni jambo lisilotamanika sababu* ***linama-anisha*** *kuwa anayeathiriwa anaipa dawa hiyo utawala juu ya hiari yake... (Oloo, 2001:1).*

Bila shaka, msomaji wa aya hii atakwama kuelewa ujumbe wa matini hii kwa sababu ya vipengele mbalimbali vilivyokozwa ambavyo havijafasiriwa kikamilifu au vimefasiriwa vibaya. Halikadhalika, msomaji atasoma kwa kusitasita ili kutafuta usahihi wa kile kinachowasilishwa. Ni vyema mfasiri au mhakiki kuwekea alama matatizo kama haya.

Uchangamano au usahili wa tungo unapaswa pia kuangaliwa kutegemeana na kiwango cha elimu cha wasomaji. Kile ambacho hadhira fulani inakiona kuwa rahisi, hadhira nyingine inaweza kukiona kigumu. Kwa mfano, hadhira ya wasomi kama vile wenye kiwango cha elimu ya chuo kikuu inaweza kusoma hata tungo changamano na kuzielewa hali ambayo ni tofauti kwa wasomaji wachanga kielimu au wanafunzi wa shule za msingi. Ndio maana wataalam wa tafsiri kama vile Larson (1984) wanapendekeza kwamba tathmini ya usomekaji ifanyike kwa kundi lengwa la matini husika. Kama matini ya tafsiri imekusudiwa kusomwa na wanasheria, basi tathmini ya usomekaji ifanyike kwa wanasheria pia. Halikadhalika, hadithi fupi za watoto zipelekwe kusomwa na watoto kwa sauti na, katika matini kama hizi mfasiri anashauriwa kutumia sentensi fupifupi.

Mbinu ya usomekaji inaweza kufanyika sambamba na mbinu nyingine kama vile za kupima uelewekaji, uasilia na ulinganifu. Kwa misingi hii, tathmini ya usomekaji itasaidia pia kurekebisha masuala mbalimbali ya kitahajia, alama za uandishi, ukubwa wa maandishi, na kadhalika. Kwa ujumla masuala yote yanayohusu uelewekaji wa maudhui, muundo na mtindo wa matini hushughulikiwa katika mchakato huu.

### 3.5 Kupima Ulinganifu

Ulinganifu hapa una maana ya umakini katika kutumia kwa namna inayofanana vipengele muhimu vya matini kama vile msamiati, istilahi au maneno muhimu yanayobeba maudhui ya matini. Mwandishi au mfasiri hapaswi kuyumba katika maneno istilahi na/au msamiati muhimu anapoiandaa matini yake. Kwa mfano, ikiwa dhana fulani ameitengenezea kisawe chake, anapaswa kutumia kisawe hicho kwa namna moja katika maeneo yote ambapo istilahi hiyo itajitokeza. Katika mchakato wa kutathmini tafsiri, pamoja na mbinu nyingine zilizoelezwa hapo juu, matini ya tafsiri pia hufanyiwa tathmini ya kupima ulinganifu wa matumizi ya vipengele muhimu kwenye matini. Hivyo, mfasiri anapokaribia ukingoni mwa zoezi lake la kutafsiri, ni muhimu sana kufanya tathmini ya vipengele muhimu vya matini yake ili kuona kama vimetumiwa kwa ulinganifu katika matini nzima au kama kuna uyumbaji wa namna yoyote. Kwa kufanya hivyo, anaweza kurekebisha aina zozote za uyumbaji katika kuhawilisha istilahi, maneno makuu yanayobeba maudhui ya matini, msamiati muhimu, na kadhalika.

Hosseini (2008) anafafanua kwamba kwa kawaida matini chanzi huwa na maneno makuu yanayobeba ujumbe au maudhui ya matini inayoshughulikiwa. Mfasiri makini, katika mchakato wa maandalizi, hubainisha maneno haya kwa lengo la kuyatafutia visawe kabla ya kuanza kufasiri. Kwa maelezo zaidi soma

pia sehemu inayozungumzia hatua mbalimbali za mchakato wa kufasiri katika Larson, (1984), Newmark, (1988) na Mwansoko na wenzie (2006). Kama muktadha hautalazimu kufanya mabadiliko yoyote yale, mfasiri anashauriwa kutumia kisawe kile kile kila mahali ambapo istilahi au msamiati huo utakapojitokeza. Malangwa (2010) anabainisha jinsi wafasiri wa programu ya *Microsoft* walivyounda visawe vya istilahi kama vile "Key – Kibonye" na "Click – bofya" na kutumia visawe hivyo kwa ulinganifu katika tafsiri zao, kama inavyojitokeza katika:

> (***Key – Kibonye***) *SHIFT key – Kibonye TEUA JUU, Shortcut key – Kibonye njia mkato* na *Tab key – Kibonye kichupo*) au (***Click – Bofya***) *Double click – Bofya mara dufu, Click on the Item selected – Bofya kwenye kipengele kilichoteuliwa* na *Right click – Bofya kulia ...*

Katika mfano huu, visawe vilivyopendekezwa vimetumika kwa ulinganifu katika mazingira yote ambamo istilahi hizo zimejitokeza. Kwa misingi hiyo, kisawe maalumu kilichoteuliwa kuwasilisha dhana fulani maalumu kinapaswa kutumika vivyo katika matini nzima.

Halikadhalika, ulinganifu unapaswa pia uangaliwe katika vipengele vya kitahajia, mfano, tahajia za majina ya watu na sehemu maalumu kama vile majina ya nchi, mikoa, majimbo, na kadhalika. Hili linahitaji utulivu na usomaji wa makini wa rasimu ya tafsiri ili kurekebisha uyumbaji wowote unaojitokeza.

## 3.6 Tafsiri Rejeshi

Tafsiri rejeshi (TR) ni mchakato wa kutafsiri matini ambayo tayari imefasiriwa katika lugha fulani (LL) na kuirejesha tena katika lugha chanzi kwa lengo la kuitathmini tafsiri hiyo. Kwa mfano, tafsiri ya awali inaweza kuwa ilitoka Kiingereza (LC) na tafsiri ikafanyika kwa mara ya kwanza katika Kiswahili (LL). Kwa hiyo, tathmini kwa njia ya tafsiri rejeshi itafanyika kutoka katika Kiswahili kwenda Kiingereza. Mbinu hii imetumika na watafiti wa masuala ya tafsiri, kama vile Fupi (2010), katika kuchunguza upotoshaji wa taarifa muhimu unaoweza kujitokeza katika tafsiri mbalimbali. Kwa kawaida, maeneo yenye matatizo hupigiwa mstari wa kubainishwa kwa alama yoyote ile katika matini zote tatu, yaani matini ya lugha chanzi (MLC), matini ya lugha lengwa (MLL) na matini ya tafsiri rejeshi (MTR). Tazama data ifuatayo, kwa mfano:

**Mfano 6:**

(a) *MLC:* *The May referendum is part **of a road map for the restoration of democracy**.*
*MLL:* *Habari zaidi zinasema upigaji kura za maoni nchini humo unaotarajiwa kufanyika mwezi Mei mwaka huu ni **moja ya njia za kuelekea katika democrasia**.*

*MTR:* *Additional news has said that the May referendum that is expected to take place in the country this year is **part of a road map towards democracy**.*

(b) *MLC:* *Mr. Zapetero thanked **jubilant supporters** for a **clear victory** ...*
*MLL:* *Bwana Zapetero amewashukuru **wapiga kura wake** kwa kumpatia **ushindi huo** ...*
*MTR:* *Mr. Zapetero thanked **his voters** for providing him with **such a victory** ...*
(Fupi, 2010:56-57)

Katika mfano huu maeneo yenye matatizo katika matini zote yamewekewa herufi za kukoza ili kuyaweka bayana kwa lengo la kuyarekebisha au kuyatolea ufafanuzi. Katika mbinu hii, MLC, MLL na MTR hulinganishwa kwa umakini mkubwa ili kubaini upotoshaji, makosa ya udondoshaji, uongezaji au upunguzaji wa taarifa muhimu za matini. Kwa mfano, katika data ya 6(a) hapo juu, MLC inaeleza kwamba upigaji wa kura za maoni ungesaidia kurejesha demokrasia lakini MLL inatoa taarifa ya upotoshaji kwamba hakukuwa na demokrasia na hivyo upigaji wa kura za maoni utasaidia kuleta demokrasia. Halikadhalika, katika data ya 6(b) vikumushi, *jubilant* na *clear* vimedondoshwa katika MLL hali inayoweza kusababisha upotoshaji wa taarifa muhimu.

Aidha, mbinu hii kama inavyojieleza ni kurejesha tafsiri husika katika LC kwa lengo la kupima ikiwa maudhui yaliyowasilishwa katika LC yamehawilishwa kwa usahihi na yanaeleweka kwa msomaji wa LL. Mtu anayefanya tafsiri rejeshi hapaswi kusoma wala kuonyeshwa MLC isipokuwa aelezwe kwamba lengo la tafsiri anayoifanya ni kuonyesha maudhui yaliyomo katika matini hiyo au kufanya tafsiri sisisi ya tungo moja moja na kuonyesha vyema maudhui yanayowasilishwa katika matini aliyokabidhiwa. Tazama mfano ufuatao wa tafsiri rejeshi ya dodoso la utafiti linalofahamika kama *15D instrument* lililoandaliwa na Harri Sintonen na kufasiriwa katika Kiswahili kwa lengo la kufanyia utafiti wa uwandani[3]:

[3] Dodoso hili liliwasilishwa na mwanafunzi wa hospitali ya Taifa, KCM ambaye alikuwa anataka kufanya utafiti wa uzamili katika masuala ya afya mwaka 2008/2009. Tafsiri ya awali ya dodoso hili ilifanywa na BAKITA na baadae dodoso hilo hilo liliwasilishwa TUKI kwa ajili ya tafsiri rejeshi, tafsiri ya pili na mjadala wa kina wa kubainisha matatizo yanayojitokeza katika tafsiri zilizotolewa kama itakavyoonekana katika mifano mingine inayohusiana na dodoso hili.

**Mfano 7:**

| **MLC YA 15D ITEM (KIINGEREZA)** **Questionnaire Title:** QUALITY OF LIFE QUESTIONNAIRE (15D) | **MLL YA 15D ITEM (KISWAHILI)** **DODOSO JUU YA UBORA WA MAISHA (15D©)** | **QUESTIONNAIRE ON QUALITY OF LIFE (15D©)** |
|---|---|---|
| **Instructions Line 1:** Please read through all the alternative responses to each question before placing a cross (x) against the alternative which best describes your present health status. | Tafadhali soma majibu yote katika kila swali kabla ya kuweka alama (X) kwenye jibu unaloona kuwa linaelezea vizuri hali yako ya kiafya kwa sasa. | Please read all the responses for each item before writing your mark (X) at the response which you think best describes your present health status. |
| Continue through all 15 questions in this manner, giving only one answer to each. | Endelea kufanya hivyo kwa maswali yote 15, ukitoa jibu moja tu kwa kila swali. | Continue marking all the 15 items that way, giving only one response for each item. |

Wakati mwingine watu wanaofanya tathmini wanaweza kutengeneza tafsiri rejeshi mbili ili waweze kuhakiki vyema ubora wa tafsiri iliyotolewa na kutoa mapendekezo ya visawe mwafaka katika LL. Tazama mfano ufuatao wa zoezi la tafsiri rejeshi lililofanyika kuhusiana na dodoso la utafiti la *15D instrument*:

**Mfano 8:**

| **MLC YA 15D ITEM (KIINGEREZA)** | **MLL YA 15D ITEM (KISWAHILI)** | **TAFSIRI REJESHI (TAFSIRI HURU) YA 15D ITEM** | **TAFSIRI REJESHI 2 YA 15D ITEM (TAFSIRI SISISI)** | **MAONI YA TAFSIRI REJESHI** |
|---|---|---|---|---|
| **QUALITY OF LIFE QUESTIONNAIRE (15D Harri Sintonen)** | **DODOSO JUU YA UBORA WA MAISHA (15D©)** | **QUESTIONNAIRE ON QUALITY OF LIFE (15D©)** | **QUESTIONNAIRE ON QUALITY OF LIFE (15D©)** | Almost all items are unchanged. |
| **Instructions Line 2:** Continue through all 15 questions in this manner, giving only one answer to each. | Endelea kufanya hivyo kwa maswali yote 15, ukitoa jibu **moja** tu **kwa kila swali**. | Continue marking all the 15 items that way, giving only **one** response for each item. | Continue to do so for all 15 questions, giving only **one** answer for each question. | It is possible to clarify "to each item or question" rather than just saying to each. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Section 1, Option 1:** I am able to walk normally (without difficulty) indoors, outdoors and on stairs. | Ninaweza kutembea vizuri (bila shida) **ndani ya nyumba, nje ya nyumba** na kwenye ngazi. | I can move comfortably (without difficulty) indoors, outdoors and in using stairs | I can walk well (without problem) inside the house, out of the house and on the stairs | Ok. But the concept of indoors and outdoors is hardly captured in the target language culture which also affected the translators. |
| **Section 1, Option 2:** I am able to walk without difficulty indoors, but outdoors and/or on stairs I have slight difficulties. | Ninaweza kutembea bila shida ndani ya nyumba, lakini nje ya nyumba na/au kwenye ngazi ninapata **shida kidogo**. | I can move comfortably indoors, although I have some difficulty outdoors and in using stairs. | I can walk without problem in the house, but I have a little problem to walk outside the house and/or on stairs. | "Slight", "little" and "some" are hardly differentiate d in Kiswahili. In other words, they have only one equivalent 'kidogo'. The back translators were also affected. |
| **Section 2, Option 2:** I can read papers and/or TV text with slight difficulty (with or without glasses). | Ninaweza kusoma magazeti na/au **ujumbe wa maandishi kwenye simu** kwa shida kidogo (nikivaa miwani au bila miwani). | I can read newspapers and/or mobile phone messages with some difficulty (with or without wearing glasses). | I can read newspapers and/or mobile phone messages with little problem (with or without spectacles). | Ok. TV texts have been changed to telephone messages due to some cultural factors which also forced the translators to follow. |

Katika mbinu hii ya tathmini, wahakiki hutengeneza safu na kuzipambanisha tafsiri rejeshi dhidi ya tafsiri na matini chanzi ili kubaini kipengele chenye matatizo. Katika mfano wetu hapo juu, vipengele vilivyobainika kuwa na matatizo vimekozwa ili kuvibainisha. Aidha, wakati mwingine kabla ya kufanya tafsiri rejeshi, matini chanzi inaweza kufasiriwa na watu wawili au zaidi. Kwa mfano, kama ni dodoso la utafiti na kwamba utafiti unahitaji umakini mkubwa, basi dodoso au hojaji inaweza kufasiriwa na watu wawili tofauti na kisha zote mbili kulinganishwa kwa lengo la kupata kilicho bora. Zoezi hili mara nyingi

huwa limekusudiwa kutengeneza tafsiri moja ambayo itakuwa bora zaidi. Wahakiki na wafasiri watazichukua matini lengwa zote na kuzisoma wakizilinganisha na matini chanzi. Wakati wa zoezi hili wahakiki na wafasiri hujadiliana na kukubaliana msamiati au neno linaloakisi kwa usahihi maudhui ya MC na kisha kuwa na safu inayoonyesha tafsiri mwafaka iliyofikiwa. Tazama data ifuatayo:

**Mfano 9:**

| MLC Item | Neno, kirai au kipengele chenye matatizo | Mgongano uliojitokeza | | Mapendekezo yaliyotolewa | Uamuzi wa mwisho |
|---|---|---|---|---|---|
| | | MLL1 | MLL2 | | |
| **Instructions Line 1:** Please read through all the alternative responses to each question before placing a cross (x) against the alternative which best describes your present health status. | Alternatives answers | Tafadhali soma **majibu yote mbadala** katika kila swali kabla ya kuweka alama (X) kwenye jibu unaloana kuwa linaelezea vizuri **hali yako ya kiafya kwa sasa**. Endelea kufanya hivyo kwa maswali yote 15, ukitoa jibu **moja** tu kwa kila swali | Tafadhali soma **majibu** yote katika kila swali kabla ya kuweka alama (X) kwenye jibu unalooana kuwa linaelezea vizuri **hali yako ya kiafya kwa sasa**. Endelea kwa maswali yote 15 kwa mtindo huo, ukitoa jibu **moja** tu kwa kila swali. | There are three alternatives for this phrase: **Majibu mbadala, majibu** and **majibu ya kuchagua**. To use "**mbadala**" would complicate the questionnaire (it is more technical to ordinary speakers of the target language) and, therefore, only "**majibu**" was preferred. | Tafadhali soma majibu yote katika kila swali kabla ya kuweka alama (X) kwenye jibu unaloana kuwa linaelezea vizuri **hali yako ya kiafya kwa sasa**. Endelea kufanya hivyo kwa maswali yote 15, ukitoa jibu **moja** tu kwa kila swali. |
| **Section 1, Option 2:** I am able to walk without difficulty indoors, but outdoors and/or on stairs I have slight difficulties. | without difficulties | Ninaweza kutembea **bila shida** ndani ya nyumba, lakini nje ya nyumba na/au kwenye ngazi ninapata shida kidogo. | Ninaweza kutembea bila ya matatizo ndani ya nyumba, lakini nje na/ au katika ngazi ninapata matatizo kidogo | **Bila shida** and **bila ya matatizo** They communicate the same message. So the target language phrases can be used interchangeably. | Ninaweza kutembea bila shida ndani ya nyumba, lakini nje ya nyumba na/au kwenye ngazi ninapata shida kidogo. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Section 1, Option 3:** I am able to walk without help indoors (with or without an appliance), but outdoors and/or on stairs **only** with considerable difficulty or with help from others. | - The use of the stress "only" is hardly captured. | Ninaweza kutembea bila kusaidiwa ndani ya nyumba (kwa kutumia au bila kutumia vifaa), lakini nje ya nyumba na/au **kwenye** ngazi ni kwa shida sana au kwa kusaidiwa na wengine **tu**. | Ninaweza kutembea bila kusaidiwa ndani ya nyumba (kwa kutumia au bila kutumia vifaa), lakini nje ya nyumba na/au **katika** ngazi **tu** kwa matatizo makubwa au kwa kusaidiwa na wengine. | The preposition **at** has more than one alternative, such as **katika, juu ya ... and kwenye**. The use of these words in the target language depends on the context. In this sentence the preposition **kwenye** is suitable than others.<br><br>The stress **tu** was agreed to be placed at the end of the sentence for the text to read smooth and meaningful than anywhere else. | Ninaweza kutembea bila msaada ndani ya nyumba (wa kutumia au bila kutumia vifaa), lakini nje ya nyumba na/au kwenye ngazi ni kwa shida sana au kwa kusaidiwa na wengine tu. |

Kama inavyoonekana katika mfano huu, kuna safu yenye matini chanzi, safu mbili zenye matini lengwa kutoka kwa wafasiri wawili (ambao kwa kawaida hawapaswi kufahamiana kabla), kuna safu ya maoni na safu ya mwisho ambayo imebeba makubaliano ya tafsiri bora au yenye ubora unaotakiwa. Hii ina maana kwamba wanapokuwa na tafsiri mbili hulazimika kutengeneza safu ya kutolea maoni au mapendekezo yanayolenga kuboresha tafsiri iliyotolewa.

Hosseini (2008) anashadidia kwamba baada ya zoezi la kufanya tafsiri rejeshi, mfasiri na mshauri wa tafsiri na/au mteja aliyewasilisha kazi yake kwa ajili ya tafsiri kwa pamoja, huzipitia matini zote mbili, yaani tafsiri ya awali na tafsiri rejeshi sambamba na matini chanzi yake. Lengo la kuzilinganisha matini hizi ni kutathmini ikiwa zina tofauti fulani kimaudhui na uzingativu wa mbinu na kanuni za tafsiri. Hapa hoja za kukosoa au kurekebisha zinaweza kupendekezwa ili kuwa na tafsiri bora zaidi. Katika hatua hii, mshauri au mfasiri wa tafsiri rejeshi anaweza kuoneshwa matini ya lugha chanzi sambamba na tafsiri zote mbili. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba katika zoezi hili si wakati wote wafasiri na wahakiki watafanikiwa kupata visawe vya tungo au maneno yote. Wakati mwingine maneno ya lugha yanaweza kuwa na maana tofauti au yasiwe na kisawe chake kabisa katika lugha nyingine. Jambo la msingi ni kujitahidi kuonesha uelewa wa maudhui yaliyomo katika tafsiri iliyotolewa.

Matini nyingi zinazopitishwa kwenye mbinu hii ya tathmini ni zile ambazo zinahusiana na utafiti, hasa kwa watafiti ambao ama wanatumia dodoso sanifu lililoandaliwa kwa madhumuni ya kutumika katika utafiti wa eneo fulani la maarifa au dodoso lililofasiriwa kwa ajili ya utafiti maalumu. Watafiti, kwa kushirikiana na wafasiri, wanapaswa kupima dodoso au hojaji zao ili kuona kama tafsiri iliyotolewa itawasaidia kupata data walizokusudia. Kwa ujumla, tafsiri rejeshi huwasaidia watafiti kupata data wanazozihitaji na kuwa na matokeo ambayo hayahitilafiani sana na yale yaliyowahi kufanyika katika lugha nyingine kwa kutumia dodoso au hojaji ileile. Tafsiri rejeshi kwa kawaida huwa ghali sana na inachukua muda mrefu na hivyo, watu wengi huwa hawaipendelei.

Mwisho ni vema kutahadhalisha kwamba kuna haja ya kuwa makini sana katika kutumia tafsiri rejeshi. Kama zilivyo mbinu nyingine za tathmini, mbinu hii ina upungufu wake. Kwa mfano, wakati mwingine mfasiri wa tafsiri rejeshi anaweza asiwe mahiri sana katika LC na LL na hivyo akatoa tafsiri rejeshi tenge kuliko tafsiri yenyewe. Wakati mwingine kwa kuwa tafsiri rejeshi hufanywa kisisisi inaweza kuwa na upotoshaji wa aina fulani na huwa haisomeki kiuasilia. Kwa ujumla, katika taasisi zinazojishughulisha na tafsiri, inafaa kuajiri mtu aliyesomea tafsiri rejeshi.

## 4.0 Hitimisho

Lengo kuu la makala haya lilikuwa kujadili mbinu mbalimbali za kutathmini tafsiri. Katika mjadala wetu tumeabiri mbinu zipatazo sita, kwa kuonesha jinsi kila mbinu inavyotumika na umuhimu wake katika kuboresha ama tafsiri au mchakato wa kutafsiri. Ni vyema tukahitimisha kwa kueleza kwamba, si kila maoni yanayotolewa katika kuhakiki au kutathmini tafsiri ni bora na yanafaa kutumika katika kuboresha zao la tafsiri. Wakati mwingine maoni yanaweza kupotosha kama Mwansoko na wenzie (2006) wanavyopendekeza kwamba ni vyema mfasiri awe makini katika kutumia mapendekezo na maoni yaliyotolewa na wasomaji, wahakiki au washauri wa tafsiri. Wakati mwingine, kama yeye amefanya utafiti wa kutosha, ataweza kuyatathmini pia maoni ya wahakiki au washauri wake na kuyafanyia kazi vizuri. Hivyo wakati mwingine wahakiki wanaweza kutoa maoni yanayopotosha na hivyo yakachangia kuharibu tafsiri itakayotolewa. Hivyo, ni vyema mfasiri awe na uelewa wa kutosha katika uwanja wa matini anayoshughulikia na kudodosa maandiko mbalimbali yanayohusiana na matini anayotafsiri au hata kwa kuongea na mteja wake ili kupunguza maswali aliyo nayo kuhusiana na matini hiyo.

**Marejeo**

*Biblia: Maandiko Matakatifu.* (1997). Nairobi: Bible Society of Kenya.

Bielsa, E. na Bassnett, S. (2009). *Translation in Global News.* Routledge: New York.

Chachage, C.S.L. (2004). "Kiswahili katika Muktadha wa Utandawazi." Katika *Kiswahili na Utandawazi.* Dar es Salaam: BAKITA. Uk. 1-17

Fupi, R. (2010). "A Critique of Electronic Media Translations: A Case Study of TBC (Television) English – Kiswahili Translations." Unpublished M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam.

Hosseini, T. S. (2008). *Ways of Testing a Translation & Testing and Evaluation in the Translation Classroom.* Katika http://www.translationdirectory.com/articles/article1699.php, ilisomwa tarehe 30, Septemba, 2010

*Indagano Inya:ya yo Mukama no Mukisya Weswe Niwe Yesu Kristo-The New Testament in Kijita, (Kikara and Kiruri)* (1960). Dodoma: The Bible Society of Tanzania.

King'ei, K. (2002). "The Challenge of Translating Poetic and Metaphoric Language from a Translation: The Case of Okot p'Bitek's *Song of Lawino.*" Katika *Metamorphoses Journal.* Massachusetts: Amherst/Northampton, Juz. 10, ukr. 152-163.

Larson, M. L. ( 1984 ). *Meaning – based translation.* Bostorn Way: University press of America.

Malangwa, P.S. (2010). "Handling Technical Translations: The Case of Translations of Computer Programs from English into Kiswahili." Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

------------------ (2008). "Ukiushi katika Kutafsiri Matini za Kifasihi: Mifano kutoka Tafsiri ya Julius Kambarage Nyerere: *Mabepari wa Venisi.*" Katika *Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI. Juz. 71, kur. 24-33.

------------------ (2005). "Problems of Translating Literary Works: The Case of Julius Kambarage Nyerere's Translation of the Play *Mabepari wa Venisi.*" Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwi), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mwansoko, H.J.M, R.D.K. Mekacha, D.L.W. Masoko na P.C.K. Mtesigwa. (2006). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu.* Dar es Salaam: TUKI.

Nida, E. na C. R. Taber .(1982). *The Theory and Practice of Translation.* Shanghai: Foreign Language Education Press.

Oloo, N.O. (2001) Kuhusu Ulevi. (Tafsiri ya About Drinking). Nairobi: Paulines Publications Africa

Pembe, H. (2010). *The Challenge of Translating Poetic Text : The Case of Paul Sozigwa's* ***Wimbo wa Lawaino***. Unpublished M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam.

*Testimenti Mpya* (The New Testament in Kinyakyusa). Dodoma, Chama cha Biblia Tanzania.

*The Holy Bible: The New International Version Containing the Old Testament and New Testament.* (2001). Great Britain: International Bible Society Great Britain Press.

Walibora, K.W. (2001). "Matatizo ya Tafsiri katika Vyombo vya Habari." Katika *Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Juz. 64, kur. 23-30.